**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2019

## 614 MAARIFA YA JAMII

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2019

## 614 MAARIFA YA JAMII

*Kimechapwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es Sa laam, Tanzania.

**©Baraza la Mitihani la Tanzania, 2019**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO


1.0 UTANGULIZI ........ 1
2.0 TATHMINI YA MAJIBU YA MTAHINIWA KWA KILA SWALI ........ 2
2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi (Taaluma) ........ 2
2.1.1 Swali la 1: Nchi yetu Tanzania ........ 2
2.1.2 Swali la 2: Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani ........ 5
2.1.3 Swali la 3: Sayari Dunia ........ 8
2.1.4 Swali la 4: Sayari Dunia ........ 10
2.1.5 Swali la 5: Sayari Dunia ........ 13
2.1.6 Swali la 6. Upinzani dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Barani Afrika ........ 15
2.1.7 Swali la 7: Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika ........ 19
2.1.8 Swali la 8: Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi Katika Afrika Huru ........ 21
2.1.9 Swali la 9: Asili na Mabadiliko ya Binadamu Teknolojia na Mazingira. ........ 24
2.1.10 Swali la 10: Ukombozi wa Bara la Afrika ........ 27
2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha (Taaluma) ........ 30
2.2.1 Swali la 11. Nchi yetu Tanzania ........ 31
2.2.2 Swali la 12: Sayari Dunia ........ 35
2.2.3 Swali la 13: Utawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika ........ 39
2.2.4 Swali la 14: Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika Zanzibar na Kwingineko Afrika. ........ 43
2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha (Ufundishaji) ........ 47
2.3.1 Swali la 15: Upimaji na Tathmini ........ 48
2.3.2 Swali la 16: Misingi ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Historia ........ 53
3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KWA KILA MADA. ........ 57
4.0 HITIMISHO ........ 58
5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ........ 59
KIAMBATANISHO ........ 60

## DIBAJI

Taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya mtihani wa somo la Maarifa ya Jamii Daraja la III A ngazi ya cheti imetayarishwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, wakufunzi, watunga sera pamoja na wadau wengine wa elimu. Mtihani ni sehemu ya upimaji wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ambayo huweza kutoa tathmini ya namna utekelezaji wa mtaala wa ngazi husika ulivyofanyika.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika taarifa hii umefanyika ili kuonesha sababu zilizofanya watahiniwa kujibu maswali vizuri au kushindwa kujibu vizuri. Uchambuzi wa kila mada na kiwango cha kufaulu katika mada husika umefanyika na sababu za mada hizo kufanyika vizuri au vibaya imebainishwa.

Uchambuzi wa majibu uliowasilishwa katika taarifa hii unaonesha kuwa watahiniwa wengi waliweza kuelewa matakwa ya maswali ya mtihani huo na hivyo kutoa majibu yaliyokidhi mahitaji ya maswali. Aidha, wapo watahiniwa wachache pia walioshindwa kujibu baadhi ya maswali vizuri, na hivyo kupata ufaulu hafifu. Sababu zilizosababisha watahiniwa hao kushindwa kujibu maswali kwa ufasaha ni pamoja na kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika, kutoelewa matakwa ya swali na kushindwa kuhawilisha maarifa ya dhana moja na nyingine. Aidha baadhi ya watahiniwa walichanganya dhana na hivyo kutoa majibu ambayo hayakuwa yamekusudiwa katika maswali husika.

Ni matarajio ya Baraza la Mitihani la Tanzania kuwa, taarifa hii itatoa mrejesho ambao utatumiwa na wadau wa elimu katika kuboresha mafunzo ya masomo ya Historia na Jiografia katika ngazi ya cheti. Baraza linatarajia pia kwamba kasoro zilizobainishwa zitashughulikiwa ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji katika Vyuo vya Ualimu. Hii itatuwezesha kutoa walimu bora wa somo la Maarifa ya Jamii na kuboresha kiwango cha ufaulu kwa walimu tarajali.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuwashukuru Maafisa Mitihani, Wakufunzi na wadau wengine wote walioshiriki katika uchambuzi wa takwimu na kuandaa taarifa hii.

Dkt Charles E. Msonde

**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa Ualimu Daraja la III A (GATCE) uliofanyika Mei 2019 kwa lengo la kutoa mrejesho kuhusu namna watahiniwa walivyojibu maswali katika mtihani wa Maarifa ya Jamii.

Mtihani wa Maarifa ya Jamii unatokana na masomo ya Jiografia na Historia yanayofundishwa katika ngazi ya cheti. Mtihani wa somo hili ulikuwa na jumla ya maswali kumi na sita (16) yaliyogawanyika katika sehemu A, B na C. Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali kumi na nne (14) ambapo sehemu A walitakiwa kujibu maswali kumi 10: Maswali matano (5) ya somo la Jiografia na maswali matano (5) ya somo la Historia. Sehemu B ilikuwa na maswali manne ya insha yaliyogawanyika katika vipengele viwili (2) kutoka katika mada za Taaluma za masomo ya Jiografia na Historia. Mtahiniwa alitakiwa kujibu swali moja kutoka katika kila kipengele cha Jiografia na Historia. Sehemu C ilikuwa na maswali mawili kutoka katika mada za ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Jiografia na Historia, na mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu hii.

Katika mtihani wa somo la Maarifa ya Jamii, jumla ya watahiniwa 4,202 walifanya mtihani na kufaulu kwa asilimia 98.50 kwa kupata daraja A hadi D na watahiniwa 63 sawa na aslimia 1.5 walishindwa kwa pata daraja F. Ufaulu wa watahiniwa katika mtihani huu umeshuka kwa asilimia 1.48, ikilinganishwa na mtihani wa mwaka 2,018 ambapo watahiniwa 4,822 walifanya mtihani na kufaulu kwa asilimia 99.98 na mtahiniwa mmoja tu alipata daraja F.

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa umegawanyika katika viwango vitatu ambavyo ni “vizuri”, “wastani” na “hafifu”. Ufaulu wa kiwango kizuri ni kuanzia alama 70 hadi 100: kiwango cha wastani ni kuanzia alama 40 hadi 69; na ufaulu wa kiwango hafifu ni kuanzia alama 0 hadi 39. Aidha, vielelezo vya viwango vya kufaulu zimeambatanishwa ili kufafanua ufaulu wa watahiniwa ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu wa kiwango kizuri, rangi ya njano inawakilisha ufaulu wa wastani na ufaulu wa kiwango hafifu unawakilishwa na rangi nyekundu.

Lengo la uchambuzi huu ni kuonesha hali halisi ya jinsi watahiniwa walivyojibu maswali katika mtihani wa Maarifa ya Jamii. Sampuli za majibu yao zimeambatanishwa ili kuonesha kilichotarajiwa kufanywa na watahiniwa

na kile kilichofanywa. Aidha, sababu za watahiniwa kujibu vizuri au kushindwa kujibu vizuri zimeanishwa. Sampuli za majibu ya watahiniwa zimetumika katika vielelezo ili kuwawezesha wadau mbalimbali kuona mifano ya hoja zilizotolewa. Hivyo, uchambuzi huu utasaidia kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Maarifa ya Jamii kwa mada ambazo zilikuwa na ufaulu hafifu ili kuinua kiwango cha ufaulu.


## 2.0 TATHMINI YA MAJIBU YA MTAHINIWA KWA KILA SWALI

### 2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi (Taaluma)

Sehemu A ya mtihani wa Maarifa ya Jamii ilikuwa na maswali 10 ya majibu mafupi, na kila swali lilikuwa na jumla ya alama nne (4). Kufaulu kwa watahiniwa katika sehemu hii kuligawanyika katika makundi matatu kulingana na alama walizopata. Watahiniwa waliopata alama kuanzia 0 hadi 1.5 walihesabika kuwa na ufaulu hafifu, ufaulu wa wastani iwapo walipata alama kuanzai 2 hadi 2.5. Aidha, watahiniwa walihesabika kuwa na ufaulu mzuri iwapo walipata alama kuanzia 3 hadi 4 katika swali husika.


#### 2.1.1 Swali la 1: Nchi Yetu Tanzania

Swali la 1 lilitoka katika mada ya *Nchi Yetu Tanzania* na lililenga kupima nyanja ya ufahamu. Swali hili lilimtaka mtahiniwa kufafanua athari za ongezeko la kasi la watu nchini Tanzania. Jumla ya watahiniwa 4,202 walijibu swali hili, na kati ya hao, watahiniwa 243 (5.8%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5, ambao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa wengine 518 (12.3%) walipata alama kuanzai 2 hadi 2.5, ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 3,442 (81.9%) walipata alama kuanzai 3 hadi 4, ambao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla, watahiniwa walifaulu swali hili kwa kiwango kizuri kwa kuwa jumla ya watahiniwa 3,960 (94.2%) walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na.1.




**Chati Na. 1:** *Viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika swali la kwanza.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa asilimia 81.9 ya watahiniwa waliopata alama kuanzia 3 hadi 4 walikuwa na ufahamu mzuri wa mada na waliweza kuelewa matakwa ya swali hili kuhusu athari za ongezeko la kasi la watu nchini Tanzania, kwa hivyo, waliweza kujibu swali hili kwa ufasaha. Baadhi ya watahiniwa waliojibu swali hili vizuri walifafanua athari hizo kama vile; *kutokea kwa vitendo vya uhalifu, kupungua kwa huduma za jamii, ukosefu wa ajira, kutokea kwa magonjwa ya kuambukiza n.k.* Kielelezo Na 1.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi na kupata alama zote nne.



1. i. Kuwepo kwa milipuko ya magonjwa. Pale ambapo kuna ongezeko la watu magonjwa yatakuwepo kwani watu huwa ni tofautitofauti.

ii. Uharibifu wa mazingira
Hii hutokea pale ambapo watu wapo wengi katika eneo moja hii hupelekea mazingira kuharibika kwani kutakuwa na utupaji wa taka ovyo.

iii. Ukosefu wa ajira
Pia kutokana na wingi wa watu itapelekea hata ajira kutokuwepo na hata zikiwepo ni kwa watu wachache sana. Hivyo kutokana na ongezeko la watu pia ajira inakosekana.


iv. Ongezeko kubwa la wahalifu/wezi; Hii pia hutokea kwani watu wamekosa kazi wanaamua kutumia mbinu zao wenyewe ili kujikimu na kujikwamua kimaisha. Hivyo kutokana na ongezeko la watu kukosa kazi hupelekea wahalifu kujitokeza kwa wingi.

**Kielelezo Na 1.1**: Kinaonesha mtahiniwa aliyeweza kufafanua kwa usahihi athari za ongezeko kasi la watu nchini Tanzania

Watahiniwa waliopata alama kuanzia 2 hadi 2.5 katika swali hili walitoa majibu ambayo hayakujitosheleza na hivyo kupata alama pungufu. Aidha, baadhi yao walichanganya majibu sahihi na mabayo hayakuwa sahihi, na wengine walitoa hoja pungufu na hivyo, kupata alama za wastani.

Watahiniwa waliopata alama kuanzia 0 hadi 1.5, walishindwa kujibu swali hili vizuri. Hali hii ilitokana na watahiniwa kushindwa kuelewa matakwa ya swali na kutokuwa na maarifa ya kutosha. Hii iliwafanya

watoe majibu ambayo hayakuendana na matakwa ya swali. Mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua sababu za ongezeko la kasi la watu kwa hoja kama vile; *kuwepo kwa ndoa za utotoni, uwepo wa chakula cha kutosha, ndoa za mitara na kukosa elimu.* Kielelezo Na 1.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vibaya.



1 ~~1. kusoa~~
i) kukosa elimu ya mpango wa uzazi hii ni kwamba watu wengi hawana elimu ya mpango wa uzazi
ii) kuwepo kwa ndoa za utotoni ni kwamba bado nchi ya tanzania kuna ndoa wengi za ututoni
iii) Uwepo wa Chakula cha kutosha ni kwamba tanzania uwepo Chakula kupelea watu kuzaliana wengi
iv) Imani za dini kwa mfano waislamu wanaamini kuoa mwisho wanawake wanne (4) kusababishwa kuongezeka kwa kasi ya watu

**Kielelezo Na 1.2**: Sampuli ya mtahiniwa ambaye hakuelewa matakwa ya swali.

### 2.1.2 Swali la 2: Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani


Swali la 2 lilitoka katika mada ya *Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani*. Swali lilikuwa na vipengele viwili; katika kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa kueleza dhana ya gridi. Katika kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kuonesha namna ambavyo mistari ya grid ni muhimu katika usomaji wa ramani na swali lililenga kupima nyanja ya maarifa. Jumla ya watahiniwa 4,202 walijibu swali hili, ambapo watahiniwa 1,452 (34.6%) walipata alama kuanzia 0 hadi1.5, ambao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa wengine 655 (15.6%) walipata alama kuanzia

2 hadi 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani, na watahiniwa 2,093 (49.8%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4, ambao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla swali hili lilikuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu, kwa kuwa jumla ya watahiniwa 2,748 (65.4%) walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Muhtasari wa kiwango cha kufaulu katika swali hilo ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na 2.




**Chati Na. 2:** *Viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika swali la pili*

Uchambuzi wa majibu unaonesha kuwa watahiniwa 2,093, sawa na asilimia 49.8 walipata alama kuanzia 3 hadi 4. wengi wao walifanya vizuri kwenye swali hili kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha juu ya Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani. Maarifa hayo yaliwasaidia kufafanua kwa usahihi dhana ya gridi kuwa *ni mistari iliyochorwa kwenye ramani kutoka mashariki kwenda magharibi na kutoka kusini kuelekea kaskazini.* Watahiniwa waliweza pia kuonesha umuhimu wa mistari ya gridi katika kusoma ramani kwa hoja kama vile; *kusaidia kutafuta mahali na kuonesha umbali kutoka eneo moja hadi lingine kwenye ramani*. Kielelezo Na 2.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.



2 a) Mistari ya gridi ni mistari inayochorwa kwenye ramani kutoka mashariki kwenda magharibi - na kutoka kusini kuelekea kaskazini.

b) i) Hutumika kuonesha mahali kwenye ramani.
ii) Hutumika katika ukokotoaji wa maeneo katika ramani.
iii) Hutumika kuonesha kuonesha umbali kwenye ramani.

**Kielelezo 2.1** Sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kufafanua dhana ya mistari ya grid na kuonesha umuhimu wake kwa usahihi.

Watahiniwa 655, sawa asilimia 15.6, walipata ufaulu wa wastani katika swali hii. Watahiniwa hawa walitoa majibu ambayo hayakujitosheleza katika baadhi ya vipengele na wengine walichanganya majibu sahihi na ambayo hayakuwa sahihi. Aidha, wangine walirudia kuandika hoja zaidi ya mara moja zenye maana moja.

Watahiniwa 1,452, sawa na asilimia 34.6, walipata ufaulu hafifu katika swali hili. Baadhi ya watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada husika na wengine walishindwa kuelewa matakwa ya swali na hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi. Mfano wa majibu ya mtahiniwa ambayo hayakuendani na matakwa ya swali ni kama vile; *umuhimu wa mistari ya gridi ni kusoma nyuzi katika ramani, kuonesha uwiano wa Ikweta moja hadi nyingine na kukokotoa muda.* Kielelezo Na 2.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha matakwa ya swali.



2. (a) Ni mistari inayochorwa katika ramani ambayo huonesha nyuzi za latutlani:-

(b)

(i) Hutumika katika kusoma nyuzi katika ramani

(ii) Hutumika kuonesha uwiano wa ikweta moja hadi nyingine.


(iii) Hutumika kukokotoa muda.

**Kielelezo Na 2.2**: Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa majibu yasiyoendana na matakwa ya swali

### 2.1.3 Swali la 3: Sayari Dunia


Swali la 3 lilitoka katika mada ya *Sayari Dunia*. Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa kueleza tofauti kati ya majanga ya kiasili na majanga ya kibinadamu. Swali hili lililenga kupima nyanja ya maarifa.

Jumla wa watahiniwa 4,202 (100%) walijibu swali hili. Watahiniwa 981 (23.3%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5, ambao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa wengine 1,394 (33.2%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani, na watahiniwa 1,827 (43.5%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla, swali hili lilifanyika vizuri kwakuwa watahiniwa 3,202 (76.7%) walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hilo ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na 3.




**Chati Na. 3:** *Viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika swali la tatu*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa waliopata alama kuanzia 3 hadi 4 walidhihirisha walikuwa na maarifa ya kuhusu ya Sayari Dunia, na waliweza kuelewa matakwa ya swali. Watahiniwa hawa waliweza kueleza vizuri tofauti iliyopo baina ya majanga ya kiasili na majanga ya kibinadamu kwa kuzingatia jinsi majanga hayo yanavyosababishwa, yanavyozuilika, dalili zake na ukubwa wa athari zake. Kielelezo Na 3.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya swali kwa usahihi.




| | |
|---|---|
| 3: Majanga ya asili | Majanga ya binadamu. |
| i. Hutokea asilia bila kusababishwa na chochote chochote Mfano. Mfuliko, kimbunga | - Husababishwa na binadamu Mfano Ajari, Machafuko ya siasa. |
| ii. Hayawezi kuepukika kwa urahisi | - Yanaweza kuepukika |
| iii. Yanaweza kuonesha dalili za kutokea kwa kutumia vipimo Mfano Mafuliko | - Hayawezi kupimwa dalili zake |
| iv. Huna na athari kwa sehemu kubwa sana | Inaweza kuathiri sehemu ndogo mfano ajari |

**Kielelezo Na 3.1:** Sampuli ya mtahiniwa aliyeweza kutoa tofauti kati ya majanga ya asili na majanga ya binadamu kwa usahihi

Watahiniwa 1,394, sawa na asilimia 33.2 walipata ufaulu wa wastani, Watahiniwa hawa walitoa majibu ambayo hayakujitosheleza katika baadhi ya vipengele na wengine walichanganya vipengele sahihi na visivyo sahihi na hivyo kupata alama za wastani katika swali hili.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 981, sawa na asilimia 23.3, walipata ufaulu hafifu. Wengi wao walishindwa kuelewa matakwa ya swali na wengine walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu Sayari Dunia. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja majanga ya kiasili kama vile *ukame, magonjwa, tetemeko la ardhi, mlipuko wa kivolkano*. Majanga ya asili ni kama vile *kukata miti uchomaji wa misitu kulima karibu ya vyanzo vya maji na uchomaji mkaa* hata hivyo hawakuonesha tofauti kati ya majanga hayo. Kielelezo Na 3:2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutofautisha majanga ya kiasili na ya kibinadamu.



| 3 | Majanga ya kiasili | Majanga ya kibinadamu |
|---|---|---|
| i/ | Ukame | Kukata miti ovyo |
| ii/ | Magonjwa | Uchomaji wa misitu |
| iii/ | Mlipuko wa kivolkano | Kulima karibu na vya |
| iv/ | ~~Tetemeko la ardhi~~ | nzo vya maji |
| v/ | Tetemeko la ardhi | Uchomaji wa mkaa |


**Kielelezo Na 3.2**: sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakuzingatia mahitaji ya swali.

### 2.1.4 Swali la 4: Sayari Dunia

Swali la 4 lilitoka katika mada ya *Sayari Dunia* na mtahiniwa alipaswa kueleza jinsi ambavyo kupatwa kwa jua na mwezi hutokea. Swali hili lililenga kupima nyanja ya uchambuzi.


Jumla ya watahiniwa 4,202 (100%) walijibu swali hili. Kati ya watahiniwa 1,156 (27.7%) walipata alama kuanzia 0 na 1.5, ambao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa wengine 1388 (33%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5, ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 1658 sawa na asilimia 39.5 walipata alama kuanzia 3 hadi 4, ambao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla katika swali hili ulikuwa na wa kiwango cha wastani.

Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na 4.




**Chati Na. 4:** *Viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katiak swali la nne*

Uchambuzi unaonesha kuwa asilimia 39.5 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 3 hadi 4 katika swali hili waliweza kutoa majibu sahihi kutokana na kuelewa matakwa ya swali. Watahiniwa hawa waliweza kueleza vizuri jinsi ambavyo kupatwa kwa jua na mwezi hutokea kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Sayari Dunia. Watahiniwa hawa waliwasilisha majibu sahihi kwa maelezo na kwa kutumia michoro. Kielelezo Na 4.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetoa maelezo sahihi yanayofafanua namna ambavyo kupatwa kwa mwezi na kupatwa kwa jua hutokea.




4. a) Kupatwa kwa jua.
Kupatwa kwa jua hutokea pale ~~dunia inapo~~ mwezi unapokuwa kati kati ya Jua na dunia na mwezi kuzuia mionzi ya jua kuweza kufikia dunia hivyo dunia huonekana kuwa giza kwa sababu ya kuto-kuwa au kukosa mwanga wa jua.

b) Kupatwa kwa mwezi
Kupatwa kwa mwezi hutokea pale dunia inapokuwa katikati ya Jua na mwezi hivyo kuzuia mionzi ya jua kuweza kufikia mwezi na kusababisha mwezi kukosa mwanga na kuonekana dehemu yenye giza.

**Kielelezo Na 4.1:** sampuli ya mtahiniwa aliyeweza kueleza kwa usahihi kupatwa kwa mwezi na kupatwa kwa jua hutokea.

Watahiniwa 1,388 sawa asiliamia 15.6%, walipata ufaulu wa wastani. Watahiniwa hawa waliweza kuelezea jinsi ambavyo kupatwa kwa jua. Baadhi yao walishindwa kuelezea kupatwa kwa mwezi na wengine walishindwa kuelezea kupatwa kwa jua.

Watahiniwa 1,156, sawa na asilimia 27.7, waliopata ufaulu wa chini katika swali hili waliweza kuelezea kupatwa kwa jua kwa usahihi lakini walishindwa kuelezea kupatwa kwa mwezi kwa usahihi. Wengine walitumia michoro kuelezea kupatwa kwa jua na kupatwa kwa mwezi. Hata hivyo, michoro hiyo haikuchorwa kwa usahihi na hivyo watahiniwa walipata alama za chini na hata wengine kupata alama 0. Sababu za watahiniwa hao kujibu vibaya swali hili ni kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana nzima na hivyo kuandika majibu yasiyokuwa sahihi. Kielelezo Na 4.2 ni sampuli ya majibu la mtahiniwa aliyetumia michoro ambayo haikuwa sahihi kuonesha kupatwa kwa jua na kupatwa mwezi.


4. Kupatwa kwa jua
Ni kitendo ambacho hutokea pale ambapo Dunia inakuwa katikati ya jua na mwezi

Likipatwa kwa jua iko ivi

(b) Kupatwa kwa Mwezi
Ni kitendo ambacho hutokea jua kuwa katikati ya Dunia na Mwezi


Hivyo jua huweza kutoa Mwanga wake kati ka mwezi.

**Kielelezo Na 4.2:** sampuli ya majibu mtahiniwa ambaye hakuweza kuelezea kwa ufasaha kupatwa kwa mwezi na kupatwa kwa jua kwa ufasaha

### 2.1.5 Swali la 5: Sayari Dunia


Swali la 5 lilitoka katika mada ya *Sayari Dunia*, na liliuliza hivi Ndege ya shirika la Emirates iliruka uwanja wa ndege wa kimataifa wa Dar es Salaam (45°mashariki) saa 11:5 alfajiri kwenda Tokyo Japan (120°) mashariki. Je, ndege hiyo ilitua huko Tokyo Japani saa ngapi?. Katika kujibu swali hili, mtahiniwa alitakiwa kukokotoa muda kwa kuonesha njia yake. Swali hili lililenga kupima nyanja ya matumizi ya maarifa.

Jumla ya watahiniwa 4202 walijibu swali hili, na kati yao, watahiniwa 1955 (46.5%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5, ambao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa wengine 1037 (24.7%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani, na watahiniwa 1210 (28.8%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla, watahiniwa walifaulu swali hili kwa kiwango cha wastani, kwa kuwa jumla ya watahiniwa 2247 (53.5%) walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Chati Na.5. inaonesha kufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 5:** *Viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika swali la tano*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa asilimia 28.8 ya watahiniwa waliweza kufanya vizuri katika swali hili kwa kuandika majibu sahihi. Hii ilitokana na kuwa na maarifa ya kutosha yaliyowawezesha kuelewa mahitaji ya swali. Watahiniwa hao waliweza kukokotoa muda kwa kutumia kanuni husika. Kielelezo Na 5.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi.




5 Njia.
- Dar es-salaam 45° mashariki saa 11:15
- Tokyo Japan 120° mashariki
Kutafuta utofauti wa nyuzi.
120° − 45° = 75°
saa 1 = 15°
? = 75°
15° × x = saa 1 × 75°
15°  15°
x = saa 5
Saa 11:15 + saa sido = 4:15
= 4:15 asubuhi.
∴ Muda huo utakuwa ni saa 4:15 asubuhi kwa saa za Japani.

**Kielelezo Na 5.1:** sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kukokotoa swali kwa usahihi

Aidha, watahiniwa 1,037 sawa na asilimia 24.7, waliopata ufaulu wa wastani, waliweza kukokotoa jibu kwa kuonyesha njia sahihi lakini hawa kukalimisha hatua zote na hivyo kupata alama za wastani.

Watahiniwa waliopata alama hafifu walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha. Watahiniwa hao walikosa ujuzi wa kanuni inayotumika katika kukokotoa muda hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitumia njia isiyokuwa sahihi hivyo akapata jibu lisilokuwa sahihi. Kielelezo Na 5.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetumia kanuni isiyokuwa sahihi katika kukokotoa muda.





**Kielelezo Na 5.2** Sampuli ya jibu lisilokuwa sahihi

### 2.1.6 Swali la 6. Upinzani dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Barani Afrika


Swali la 6 lilitoka katika mada ya *Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Barani Afrika.* Swali hili lililenga kupima nyanja ya ufahamu. Mtahiniwa alitakiwa kuchambua kwa ufupi mafunzo manne yaliyotokana na vita walivyopigana na Watanganyika dhidi ya uvamizi wa wakoloni wa Kijerumani.

Jumla wa watahiniwa 4,202 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Watahiniwa 2,283 sawa na asilimia 54.4%, walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5. Kati yao watahiniwa 1,662 sawa asilimia 39.6, walipata alama 0 ambao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa wengine 580, sawa na asilimia 14.1, walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 ambao ni ufaulu wa wastani, na watahiniwa 1,329 sawa na asilimia 31.6, walipata alama kuanzia 3 hadi 4, ambao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwa kuwa asilimia 45.6 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na 6.




**Chati Na. 6:** *Viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika swali la sita*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 2,283 sawa na asilimia 54.0, walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5. Hali hii ilitokana na kushindwa kuelewa matakwa ya swali pamoja na kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Barani Afrika. Kwa mfano mtahiniwa mmoja katika swali hili alieleza madhara yaliyotokana ya vita hiyo kama vile*; vifo, njaa, kuporomoka kwa uchumi, kuvunjika na kusambaratika kwa baadhi ya familia* badala ya kueleza mafunzo yanayopatikana katika vita hivyo. Aidha asilimia 14.7% ya watahiniwa walichanganya majibu sahihi na ambayo sio sahihi jambo ambalo lilisababisha kupata alama hafifu. Kielelezo Na 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuelewa muktadha wa matumizi ya dhana ya mafunzo manne yaliyotokana na vita walivyopigana na Watanganyika dhidi ya uvamizi wa wakoloni wa Kijerumani. Hivyo, aliandika majibu yasiyoendana na matakwa ya swali kama vile; *mafunzo ya ufundi seremala, mafunzo ya ukalani, mafunzo ya cherehani na ujenzi wa nyumba*.


SEHEMU A

6. Yafuatayo ni mafunzo yaliyotokana na vita vilivyopiganwa na Watanganyika dhidi ya uvamizi wa wakoloni wa Kijerumani.

(i) Mafunzo ya ufundi seremala. Wakoloni walipikita na ukogi wa mafunzo ya useremala.


(ii) Mafunzo ya ukalani. Pia katika makambi ndogo ndogo walipikita na mafunzo ya ukalani.

(iii) Mafunzo ya ufundi cherehani au fundi nguo. Mafunzo haya yalitelewa na Wajerumani.

(iv) Mafunzo ya ujenzi wa nyumba na kutengeneza barabara mbalimbali.

**Kielelezo Na 6.1:** Sampuli ya majibu yasiyokuwa sahihi.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha watahiniwa 1,329, sawa na asilimai 31.6 walipata alama kuanzia 3 hadi 4. Watahiniwa hawa waliweza kuchambua kwa usahihi mafunzo manne yaliyotokana na vita walivyopigana na Watanganyika dhidi ya uvamizi wa wakoloni wa Kijerumani. Wathiniwa hawa walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha na walielewa vema matakwa ya swali. Watahiniwa hao pia waliweza kuchambua mbinu zilizotumika katika kuwapa hamasa wapigania uhuru dhidhi ya wavamizi wa Tanganyika kwa hoja kama vile: *umoja ni nguvu utengano ni udhaifu, usaliti huleta matokeo mabaya katika vita, maandalizi mazuri huleta matokeo mazuri na ushindi na kutumia mbinu za kisasa katika mapigano*. Kielelezo Na 6.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


6. kwa kifupi, ~~ch~~ Mafunzo Manne yaliyotokana na vita vilivyopiganwa na waTanganyika dhidi ya uvamizi wa wakoloni wa kijerumani.

i) umoja ni nguvu utengano ni udhaifu ~~nto~~ jamii nyingi za kiafrika zilikuwa hazina umoja kila jamii ilipigana kivyake hali ambayo ilipelekea kushindwa ~~kt~~ katika vita mfano, jamii ya wahehe, wachaga, wanyamwezi.

ii) usaliti huleta matokeo mabaya katika vita mfano mangi sina na mangi mandala walisalitiana hali ambayo ilipelekea kushindwa katika vita.

6. iii) Maandalizi mazuri katika vita huleta matokeo mazuri na ushindi, kutokana na maandalizi mabaya ya waafrika ilipelekea kushindwa hivyo wangefanya maandalizi wangeweza kufanikisha na kupata matokeo mazuri

**Kielelezo Na 6.2:** Sampuli ya majibu sahihi


Kielelezo Na 6.2 Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza kwa usahihi mafunzo yaliyotokana na vita walivyopigana na Watanganyika dhidi ya ujio wa wakoloni wa kijerumani.

Watahiniwa 580, sawa na asilimia 14, waliopata ufaulu wa wastani walitoa majibu ambayo hayakujitosheleza kulingana na matakwa ya swali hili. Aidha, baadhi yao walirudia hoja zaidi ya mara moja, na hivyo kuwafanya kupata alama za wastani.

### 2.1.7 Swali la 7: Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika

Swali la hili lilitoka katika mada *ya Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika*. Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa kuchanganua kwa kifupi matokeo manne ya mkutano wa Berlin uliofanyika mwaka 1884/1885. Swali hili lililenga kupima nyanja ya uchambuzi.


Jumla ya watahiniwa 4,202 (100%) walijibu swali hili, ambapo watahiniwa 1,131 (26.9%) walipata alama kati ya 0 hadi 1.5, ambao ni ufaulu hafifu. Pia watahiniwa 1,332 (31.7%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5, ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 1739 (41.4%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla, swali hili lilifanyika vizuri. Jumla ya watahiniwa 3071 (73.1%) walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na.7.




**Chati Na. 7:** *Viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika swali la saba*

Uchambuzi wa majibu ulionesha kuwa watahiniwa 3,071, sawa na asilimia 73, walipata ufaulu mzuri katika swali hili kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika. Hii iliwawezesha kuelewa kwa ufasaha mahitaji ya swali. Watahiniwa hao waliweza pia kuelezea vizuri matokeo matatu hadi manne ya mkutano wa Berlin kama vile;

*kugawanywa kwa bara la Afrika, Mfalme Leopard wa Ubeligiji kupewa eneo la mto Kongo, kufungua mipaka katika makoloni pasipo masharti magumu, maeneo kama vile mto Kongo, Misri kuwekwa huru kwa kila mkoloni kuweza kupita katika eneo hilo bila kuzuiliwa*. Kielelezo Na.7.1 ni sampuli ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.




7. (i) Kugawanywa kwa bara la Afrika kwa usawa na kutatua migogoro iliyokuwepo.
(ii) Mfaulme leopard wa Kongo kupewa eneo la mtoto Kongo ilokuwa likipiganiwa.
(iii) Kufungua mipaka ya kibiashara koloni mmoja kuingia sehemu nyingine pasipo masharti magumu
(iv) Maeneo muhimu kama vile mto Kongo, misri na Mazwa ili fungulia ili kuweka uhuru wa kupita sehemu yeyote na kuingia kufanya biashara pasipo vizuizi vyovyote.

**Kielelezo Na 7.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la saba

Watahiniwa 1,333 sawa na asilimia 31.7 waliopata ufaulu wa wastani walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi kama; *kufungua mipaka katika makoloni pasipo masharti magumu, maeneo kama vile mto Kongo*. Majibu yasiyo kuwa sahihi ni kama *Ujerumani kulipa fidia kwa Uingereza na Zanzibar kupewa sultani Sayyid Said*. Wangine walirudia kuandika hoja zaidi ya mara moja zenye maana moja na hivyo kuwafanya kupata alama za wastani katika swali hili.

Watahiniwa 1,131, sawa na asilimia 26.9, walikuwa na ufaulu hafifu. Kati yao watahiniwa 287, sawa na asilimia 6.8, walipata alama 0 kwa sababu walitoa majibu yasiyoendana na matakwa ya swali kama vile; *Ujerumani kuachia baadhi ya makoloni, Uingereza kushikilia makoloni aliyoyaacha mjerumani, Ujerumani kulipa fidia kwa Uingereza na Zanzibar kupewa sultani Sayyid Said wa Zanzibar*. Majibu haya yalionesha matokeo ya vita kuu ya kwanza ya dunia 1914-1918. Watahiniwa wengine wailielezea hoja walizotumiwa wakoloni kuanzisha na kuimarisha uchumi wao barani Afrika kama vile; *kuanzishwa kwa kodi, kuanzishwa kwa mfumo wa fedha na kuanzishwa*

*kwa kilimo*. Kielelezo Na 7.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi, na hivyo kupata alama 0.


7. (i) Kuanzishwa kwa Mfumo wa fedha kutokana na kila koloni / taifa la ulaya kupata koloni la kutawala Afrika.
(ii) Kuanzishwa kwa kodi; kutokana na kila taifa kupata koloni la kutawala Afrika.
(iii) Kuanzishwa kwa shughuli za kilimo; kutokana na kila taifa kupata koloni la kutawala Afrika.
(iv) Kuanzishwa kwa Mashamba ya walowezi; kutokana na Mataifa ya ulaya kupata Maeneo ya kutawala Afrika.


**Kielelezo Na 7.2:** Sampuli ya majibu yasiyokuwa sahihi

## 2.1.8 Swali la 8: Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi Katika Afrika Huru

Swali la 8 lilitoka katika mada ya *Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi*, na lililenga kupima nyanja ya ufahamu. Mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa ufupi changamoto nne za upatikanaji wa huduma za kijamii kwa wananchi katika nchi za Afrika baada ya uhuru.


Jumla ya watahiniwa 4,202 (100%) walijibu swali hili. Kati yao watahiniwa 518, sawa na asilimia 13.5, walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5, ambao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa 591, sawa na asilimia 14.1, walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5, ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 3043, sawa na asilimia 72.4, walipata alama kuanzia 3 hadi 4 ambao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla, watahiniwa walifaulu vizuri katika swali hili kwa kuwa asilimia 86.5, kati ya watahiniwa wote

walipata ufaulu kuanzia alama 3 hadi 4. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na 8.




**Chati Na. 8:** *Viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika swali la nane*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 3,043, sawa na asilimia 72.4, walijibu vizuri swali hili kutokana na kuelewa matakwa ya swali na kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu changamoto za upatikanaji wa huduma za kijamii katika nchi za kiafrika baada ya uhuru. Baadhi ya changamoto huzi ni kama kama vile*; uhaba wa wataalamu, miundo mbinu mibovu na ukosefu wa fedha.* Kielelezo Na 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


8 -> Uhaba wa watalamu katika huduma za afya. hii imetokana na kukosa wataalamu wa kutosha mfano manesi, madaktari.

-> Uhaba wa vifaa mahospitalini kwa ajili ya matibabu. Kutokana na kuwa na uchumi mdogo baada ya uhuru

-> Miundo mbinu mibovu. hii imesababishwa na Vita vya mwamzo kabla ya uhuru na baada ya uhuru imekuwa changamoto mfano majengo, shule, na barabara pamoja na reli


-> Ukosefu wa fedha za kuendesha huduma za jamii. hii imetokana na baada ya uhuru nchi nyingi za kiafrika zilikuwa masikini na zilikuwa na uchumi tegemezi.

**Kielelezo Na 8.1:** Sampuli ya mtahiniwa aliyezingatia mahitaji ya swali.

Aidha, watahiniwa 591 sawa na asilimia 14.1 walipata ufaulu wa wastani, walitoa majibu machache ambayo hayakujitosheleza kulingana na matakwa ya swali. Mfano ni *miundo mbinu mibovu*. Baadhi yao pia walitoa majibu ambayo hayakuwa sahihi; kama *upatikanaji wa shule vifaa vya shule* na hivyo kupata alama za wastani.

Watahiniwa 518, sawa na asilimia 13.5, ya watahiniwa, wote walipata alama hafifu katika swali hili kutokana na kukosa umakini katika kubainisha matakwa ya swali hili. Wengine kati yao walionekana kutokuwa na maarifa kabisa kwani walieleza mambo ambayo hayana uhusiano na swali na hivyo kupata alama 0. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile; *upatikanaji wa shule, hospitali na maji* ambazo hazikuwa na uhusiano na swali. Wengine pia walichanganya majibu sahihi na ambayo hayakuwa sahihi. Kielelezo Na 8.2 ni sampuli

ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa majibu ambayo hayakuwa sahihi katika swali hili.



8 (i) ~~shule~~ upatikanaji wa shule kwa sababu shule zilikuwa na chache na walivumehwa wazungu na baadhi ya waafrika.

(iii) upatikanaji wa hospitali.


(v) Maji

**Kielelezo Na 8.**2: sampuli ya mtahiniwa ambaye alitoa hoja zisizoendana na matakwa ya swali.

### 2.1.9 Swali la 9: Asili na Mabadiliko ya Binadamu Teknolojia na Mazingira


Swali la 9 lilitoka katika mada ya *Asili na Mabadiliko ya Binadamu Teknolojia na Mazingira.* Mtahiniwa alitakiwa kutofautisha mabadiliko ya kimaendeleo wakati wa zama za mawe na wakati wa zama za chuma. Swali lilenga kupima nyanja ya maarifa.

Jumla ya watahiniwa 4,202 (100%) waliojibu swali hili. Watahiniwa 1,346 sawa na asimilia 32%, walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5 ambao ni ufaulu hafifu. Pia watahiniwa 136, sawa na asilimia 32.6, walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5, ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 1,487(35.4%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4 ambao ni ufaulu mzuri. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa kiwango cha wastani kwa kuwa jumla ya watahiniwa 2,856 sawa na asilimia 68, walipata alama 2 hadi 4. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na.9.




**Chati Na. 9:** *Viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika swali la tisa*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unabainisha kuwa watahiniwa walipata alama kuanzia 3 hadi 4 unaonesha kuwa watahiniwa hawa waliweza kutofautisha mabadiliko ya kimaendeleo wakati wa zama za mawe na wakati wa zama za chuma. Watahiniwa hao pia walidhihirisha maarifa ya kutosha na walielewa mahitaji ya swali. Baadhi ya majibu sahihi ya watahiniwa waliojibu vizuri swali hili yalionesha tofauti iliyokuwepo kwa kuzingatia vipengele kama vile; *zana zilizotumika, makazi, shughuli za kibiashara na mgawanyo wa kazi* katika zama hizo. Kielelezo Na.9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.




9. Tofauti ya Mabadiliko ya kimaendeleo wakati wa zama za mawe na zama za chuma

| | Zama za Mawe | Zama za Chuma. |
|---|---|---|
| i. | Hawakuwa na makazi ya kudumu waliishi kwa kuhamahama | - Makazi yao yalikuwa ya kudumu. |
| ii. | Walifanya kazi kwa kushirikiana hapakuwa na mgawanyo wa kazi | - Walikuwa wakigawana kazi za kufanya. |
| iii. | Zana/vifaa vyao vilikuwa duni mfano mawe na fimbo | - Vifaa/zana zao zilikuwa imara mfano Jembe, shoka, mshale. |
| iv. | Hapakuwa na shughuli za biashara ya aina yoyote | - Kulikuwa na biashara mfano. kubadilishana bidhaa kwa bidhaa au vitu. |

**Kielelezo Na 9.1**: Sampuli ya majibu sahihi.

Watahiniwa waliopata alama za wastani (2 hadi 2.5) walitoa tofauti chache na nyingine hazikuwa tofauti sahihi kwa kuwa walitoa majibu ambayo hayaoneshi tofauti iliyopo kati ya mabadiliko ya kimaendeleo wakati wa zama za mawe na wakati wa zama za chuma.

Kwa upande wa watahiniwa waliopata alama hafifu, watahiniwa 156 (3.6%) walipata alama 0 kutokana na kukosa maarifa ya kutosha katika mada hii na hivyo kushindwa kabisa kutofautisha mabadiliko ya kimaendeleo wakati wa zama za mawe na wakati wa zama za chuma. Watahiniwa wengine katika kundi hili waliopata alama kuanzai 1 hadi 1.5, walichanganya majibu yaliyokuwa sahihi na yasiyo sahihi kama inavyonekana katika Kielelezo Na 1.18, chenye sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutofautisha kwa ufasaha mabadiliko ya kimaendeleo wakati wa zama husika.




| | | |
|---|---|---|
| 9. | Zama za mawe | Zama za chuma |
| | i) Zama za mawe binadam u aliweza kugundua chuma | i) Alishagundua chuma hivyo alitumia |
| | ii) Hakugundua zana zaidi | ii) Aliweza kutengeneza zana nyingi kama shoka |
| | iii) Bado alikuwa hajaimari ka kula nyama iliyoiva | iii) Alikula nyama ya kuchoma |
| | iv) Aliwinda kwa mawe. | iv) Aliwinda kwa vyuma |

**Kielelezo Na.9.2** Sampuli ya majibu yasiyokuwa sahihi

### 2.1.10 Swali la 10: Ukombozi wa Bara la Afrika

Swali la 10 lilitoka katika mada ya *Ukombozi wa Bara la Afrika*; na lililenga kupima nyanja ya ufahamu. Mtahiniwa alitakiwa kueleza sababu zilizowafanya wananchi wa Tanganyika kuungana katika kudai uhuru.

Jumla wa watahiniwa 4,202 walijibu swali hili; kati yao, watahiniwa 483, sawa na asiliamia 1.5, walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5, ambao ni ufaulu hafifu. Pia watahiniwa 277, sawa asilimia 6.6, walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5, ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 3,440 sawa na asilimia 81.9, walipata alama kuanzia 3 na 4, ambao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla, ufaulu wa swali hili ulikuwa wa kiwango kizuri kwa kuwa jumla ya watahiniwa 3,717, sawa na asilimia 88.5, walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na.10.




**Chati Na. 10:** *Viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika swali la kumi*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 3,440, sawa na asilimia 81.9, waliopata alama kuanzia 3 hadi 4, walikuwa na maarifa ya kutosha. Baadhi ya hoja sahihi walizozitoa ni kama; *Watanganyika kuchoshwa na uongozi wa kikatili na unyonyaji uliofanywa na wakoloni, walihitaji kuachiwa ardhi yao, kulinda mila na desturi zao, walichoshwa na kutozwa kodi na kulipwa ujira mdogo pia walitaka kujitawala wenyewe n.k.* Kielelezo Na 10.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

10.

Sababu zilizowafanya wananchi wa Tanganyika kuungana katika kudai uhuru wao ni;

Kunyanganywa ardhi yao yenye rutuba, wananchi wa Tanganyika waliungana katika kudai uhuru wao kwa sababu walichukuliwa ardhi yao yenye rutuba.

Kuvunjwa kwa tamaduni zao, hii pia ni sababu iliyopelekea wananchi wa Tanganyika kuungana kwa pamoja kudai uhuru kwa sababu wakoloni walihanibu tamaduni zao.

Ulipaji wa kodi, hapa wananchi wa Tanganyika waliungana kwa pamoja kwa sababu ya kulipishwa kodi, kwani waliwafanyisha kazi nyingi na kuwalipa pesa kidogo ambayo haikuweza kukidhi mahitaji yao tena wakawalipisha walipe kodi ya kichwa, matiti.

Unyonyaji, pia waliungana kwa pamoja baada ya kuona unyonyaji unazidi kwani walikuwa wakapigwa, wanachukuliwa kuwa watumwa kwa hiyo manyanyaso yalizidi na kuamua kuungana kwa pamoja kudai uhuru wao.


Hizo ndo sababu zilizowafanya wananchi wa Tanganyika kuungana kwa pamoja katika kudai uhuru wao.

**Kielelezo Na 10.1**: Sampuli ya majibu sahihi

Watahiniwa 277, sawa na asilimia 6.6, walipata ufaulu wa wastani. Baadhi yao walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na wengine walitaja hoja zenye majibu sahihi lakini hawakuzifafanua vizuri.

Kwa upande mwingine watahiniwa 483, sawa na asiliamia 11.5, walipata alama kati ya 0 hadi 1.5. Watahiniwa waliopata alama kuanzia 1 hadi 1.5 hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya ukombozi wa Bara la Afrika. Baadhi yao walitoa hoja moja sahihi zisizo sahihi. Aidha, watahiniwa 288(6.9%) walipata alama 0 ambazo zinathibitisha kuwa walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Wengine walieleza sababu zilizokuwa nje ya Afrika na jinsi zilivyochangia Waafrika kudai uhuru kama vile; *mchango wa Marekani, mchango wa Urusi, mchango wa Waafrika weusi walioshiriki katika vita vya pili vya dunia na umoja wa wananchi Tanganyika*.

Watahiniwa wengine walitaja sababu tofauti; kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile; *huduma za kijamii, huduma za kisiasa, huduma za kiuchumi na huduma za kiutamaduni* lakini alishindwa kuzifafanua jinsi zilivyochangia wananchi wa Tanganyika kuungana katika kudai uhuru. Kielelezo Na 1.20 ni sampuli ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa kutaja sababu bila kueleza namna zilivyochangia Watanganyika kuungana kudai uhuru.


10 i/ Huduma za kijamii
ii/ Huduma za kisiasa
iii/ Huduma za kiuchumi
iv/ Shughuli za kiutamaduni

**Kielelezo Na 10.2:** Sampuli ya majibu yasiyokuwa sahihi.

## 2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha (Taaluma)


Sehemu hii ilikuwa na maswali manne yaliyogawanyika katika vipengele viwili; kipengele cha Jiografia na Historia Mtahiniwa alitakiwa kujibu swali moja (1) kutoka katika kila kipengele. Kila swali katika sehemu B lilikuwa na alama 15. Kufaulu kwa watahiniwa katika sehemu hii kuligawanyika katika makundi matatu 3 kulingana

na alama walizopata watahiniwa. Watahiniwa waliopata alama kuanzia 0 hadi 5.5 walihesabika kuwa na ufaulu hafifu, kufaulu wa wastani iwapo walipata alama kuanzia 6 hadi 10 na watahiniwa waliopata alama kuanzia 10.5 hadi 15 walihesabika kufaulu mzuri.

### 2.2.1 Swali la 11. Nchi Yetu Tanzania

Swali la 11 lilitoka katika mada ya *Nchi Yetu Tanzania* na lilimtaka mtahiniwa kubainisha mambo manne yanayoathiri tabia ya nchi.


Jumla ya watahiniwa 2,801 sawa na asilimia 66.7 walijibu swali hili, watahiniwa 1,386 sawa na asilimia 49.5, walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5, ambao ni ufaulu hafifu. Pia watahiniwa 887, sawa na asilima 31.6, walipata alama kuanzia 6 na 10 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 528, sawa na asilima 18.9, walipata alama kati ya 10.5, na 15 ambao ni ufaulu mzuri. Ufaulu wa watahiniwa ulikuwa wa kiwango cha wastani, jumla ya watahiniwa 1,415, sawa na asilimia 50.5%), walipata alama kuanzia 2 hadi 4. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali ni kama inavyoonekana kwenye Chati Na.11.




**Chati Na. 11:** *Viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 11*

Uchambuzi wa majibu unaonesha kuwa ya watahiniwa waliopata alama hafifu (0 hadi 1.5) walishindwa kuelewa matakwa ya swali; na wengine walidhihirisha kutokuwa na maarifa ya kutosha. Hii ilisababisha kutoa majibu ya kubuni na hivyo kupata alama hafifu. Kwa mfano mtahiniwa mmoja kupata alama 0 kwa mfano mtahiniwa mmoja alibainisha hoja kama vile; *tetemeko la ardhi, mafuriko, ukame*

*na kimbunga*. Wengine pia walibainisha shughuli za kibinadamu zinazoweza kuathiri tabia nchi, kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja ; *maendeleo ya viwanda, ukosefu wa mvua, ukataji miti na ongezeko la watu*. Kielelezo Na 11.1 ni sampuli ya mtahiniwa aliyetoa majibu yasiyo sahihi.


11. Tabia ya nchi; taarifa zinazorekodiwa
na kutolewa tafsiri kuhusiana na hali ya hewa
ya mahali kama kuwa na baridi au joto la
wastani, kuwa na kiasi cha mvua na unyevu.
Kuna mambo mbalimbali ambayo yanaweza
kuathiri tabia ya nchi, nayo ni kama
yafuatayo;
Maendeleo ya viwanda; ongezeko ku-
bwa la viwanda katika nchi linaweza kupelekea
tabia ya nchi kubadilika kwa sababu viwanda

11 kutoa moshi na kuelekeza angani, ambao huweza kupelekea kuongezeka kwa joto la mahali kwa mfano Dar es Salaam kuna joto kali kwa sababu ya uwepo wa viwanda vingi.

Ukosefu wa mvua; Ukame huweza kubadili tabia ya nchi ya mahali kwa sababu kutokana na mvua uoto wa asili huweza kustawi na hata hali ya hewa huwa nzuri tofauti na sehemu yenye ukosefu wa mvua za kutosha.

Ukataji wa miti au uharibifu wa misitu; misitu husaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza kwa tufani na kimbunga. Hivyo kama eneo litakuwa jangwa huweza kupelekea kuwa na upepo mkali na kimbunga mara kwa mara katika eneo hilo.

Ongezeko la watu; idadi kubwa ya watu katika eneo moja huweza kupelekea eneo hilo kuwa na mgandamizo mkubwa wa hewa na hivyo kusababisha joto / baridi katika eneo husika kuwa kali mno.

Kwa kuhitimisha, tabia ya nchi ya mahali huwa na vipengele kama vile joto au baridi, mvua, unyevu, mgandamizo wa hewa vitu ambavyo hupelekea kuongezeka kwa utalii na kupata mvua za kutosha.

**Kielelezo Na 11.1**: Sampuli ya majibu ya mtahiniwa mbaye alitoa majibu yasiyoendana na matakwa swali.

Watahiniwa 528, sawa na asilimia 18.9, walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya mambo yanayoathiri tabia nchi na hivyo waliweza kubainisha matakwa ya swali hili kwa usahihi. Watahiniwa hao waliweza kuelezea mambo manne yanayoathiri tabia nchi kwa hoja kama vile; *mwinuko kutoka usawa wa bahari, umbali kutoka usawa wa bahari, upepo, mkondo wa bahari na shughuli za binadamu*. Kielelezo Na 11.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

11. Tabia nchi Ni wastani wa hali ya hewa iliyorekodi-
wa kwa kipindi cha muda mrefu (kuanzia miaka Thel-
athini). Tabia ya nchi huchukua muda mrefu kukusanya
Taarifa zake. Mambo ambayo yanaweza kuathiri Tabia
ya nchi ni kama yafatayo:-
Mwinuko kutoka Usawa wa Bahari:- Hii hutokea
na kuathiri tabia ya nchi. Joto ndi la mahali palipo karibu
na Bahari linaongezeka na kupungua nguzi joto 0.6°c
kwa kila meta 100 kutoka usawa wa Bahari. Hivyo
tabia ya nchi huathiri na joto ndi la mahali, Ambapo lina-
kuwa linabadilika mara kwa mara.
Mkondo Bahari:- Mikondo Bahari ipo ya aina mbili
ambayo ni mikondo baridi na nyingine ni mkondo joto.
Mkondo Bahari joto husababisha kufanyika kwa mvua
hiiyo maeneo mengi yaliyo karibu na Bahari huwa nam-
vua nyingi sana kuliko maeneo mengine ambayo-
yapo mbali na Bahari. Mfano maeneo yote ya Pwani ya-
Afrika mashariki huwa na Mvua nyingi sana kila mwaka-
kuliko maeneo mengine.
Umbali kutoka Usawa wa Bahari:- Umbali kutoka-
usawa wa Bahari, watu ambao wanaishi karibu na B-
ahari hupata joto sana kuliko watu ambao wanaishi m-
bali na Bahari. Mfano Watu wanaoishi Dar es salaam
u ni tofauti na wale watu ambao wanaishi Dodoma na
Singida.
Upepo:- Ni hewa iliyo katika hali ya mwendo.
Zipo aina mbili za pepo ambazo huvuma katika pwa-
ni ya Afrika Mashariki, pepo hizo ni pepo za kusi na pe-
po za kasi. Hizi ndizo pepo maarufu zinazo vuma Pwani
ya Afrika mashariki. Hivyo Jua la utosi linapokuwa katika
Tropiki ya kansa, kizio cha kaskazini huwa na joto san
a hivyo pepo za kusi huvuma na kuelekea kwenye-

11. Kizio cha kaskazini, Lakini pia jua la utosi linapokuwa.
kwenye Tropiki ya kaprikoni ncha ya kusini huwa na joto
sana hivyo pepo za kasi huvuma kuelekea kusini.
Hivyo, hayo ni baadhi tu ya mambo ambayo yanaweza
kuathiri tabia nchi ya mahali, Lakini mambo hayo hayawe
zi kuzuilika mara yanatokea kama Asili.


**Kielelezo Na 11.2:** Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubainisha mambo yanayoathiri tabia nchi kwa usahihi.

Watahiniwa 887, sawa na asilima 31.7, walipata ufaulu wa wastani. Watahiniwa wengi katika kundi hili walielezea hoja pungufu kwa kutaja hoja kama vile; *upepo na shughuli za binadamu* na wengine walibanisha hoja ambazo hazikuwa sahihi.

### 2.2.2 Swali la 12: Sayari Dunia

Swali la 12 lilitoka katika mada ya *Sayari Dunia* na lililenga kupima nyanja ya uchambuzi. Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kueleza hatua tano zinazoweza kuchukuliwa ili kupunguza athari ikiwa janga la asili litatokea.

Jumla ya watahiniwa 1,408, sawa na asilimia 33.5, waliochagua kujibu swali hili. Kati yao watahiniwa 131, sawa na asilimia 9.3, walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5, ambao ni ufaulu hafifu. Pia watahiniwa 821, sawa na asilimia 58.3, walipata alama kati ya 6 hadi 10, ambao ni ufaulu wa wastani. Watahiniwa 456, sawa na asilimia 32.4, walipata alama kuanzia 10.5 hadi 15, ambao ni ufaulu mzuri. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa kiwango kizuri, kwa kuwa jumla ya watahiniwa 1,277, sawa na asilimia 90.7, walipata alama kuanzia 6 hadi 15. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na.12.




**Chati Na. 12:** *Viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 12.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa asilimia 88.3 ya watahiniwa waliweza kueleza hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kupunguza athari ikiwa janga la asili litatokea. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana nzima ya majanga ya asili na walielewa vema matakwa ya swali. Watahiniwa waliweza kutoa hoja sahihi kama vile: *kutoa elimu kwa jamii*, *kuunda kikundi cha kuchunguza mabadiliko ya hali ya hewa kuwa na vyombo*


*vya habari, kuboresha miundo mbinu na kuweka akiba ya chakula n.k.* Kielelezo Na 12.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi.

12 Majanga ya asili ni jumla ya matukio ambayo hayasababishwi na shughuli za binadamu mfano kibunga, Tetemeko la Ardhi, Mafuriko pamoja na Tsunami hivyo majanga haya hutokea kwa sababu za kijografia mfano Sunami huweza kusababishwa na volkano milipuko ya volkano pamoja na kutonesha kwa vimondo angani. Zifuatazo ni hatua tano ambazo zinaweza kuchukuliwa na jamii ili kupunguza athari ikiwa janga asili linatokea.

Hatua ya kwanza kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara ya majanga, Jamii inapaswa kupewa elimu kwanza kuhusu madhara ya majanga hayo mfano kibunga baada ya kutokea kibunga huweza kuathiri nyumba kwa kuezuliwa mabati pamoja na miundombinu kuharibika.

Hatu ya pili kuunda kikundi cha kuchunguza mabadiliko ya hali ya hewa, Jamii inapaswa kuwa na kikundi ambacho kitawezesha kutoa habari ambazo zinaendelea mfano watabiri wa hali ya hewa hewa ~~tutawatumia~~ watumika kuchunguza kwa makini mabadiliko ya hali ya hewa mfano mawingu, mvua, upepo na kadhalika.

Hatua ya tatu kuwa na vyombo vya habari, Hatua hii ni nzuri sana kuwa na vyombo ambavyo vitatumika katika kupasha habari kuhusu yale ambayo yatatokea baadaye kuhusu hali ya hewa mfano redio, Television.


12 Hatua ya nne kuboresha miundo-
Mbinu katika jamii, inapaswa jamii kuweza
kuboresha miundo Mbinu Mfano barabara
ambazo zitakuwa na mitaro ambayo ita
tumika katika kupitisha maji endapo janga
la mafuriko litatokea.
Hatua ya tano kuweka akiba-
ya chakula, Hatua hii ni kwa jamii ina-
paswa kutunza chakula ambacho kitaweza
kuwa msaada pindi litokeapo janga la
asili kwaajili ya kutumika katika vikundi
ambavyo watajihifadhi.
Kwahiyo Majanga ya asili huwe
za kurudisha maendeleo ya nchi kwa -
kupoteza nguvu kazi Mfano watu lakini pia
huweza kusababisha njaa Mfano wa janga
Ukame ni vyema kuwa na vitu vya ulinzi
wa hali ya hewa.

**Kielelezo Na 12.1:** Sampuli ya majibu sahihi.

Watahiniwa 456, sawa na asilimia 32.4, walipata ufaulu wa wastani. Watahiniwa hawa waliweza kueleza hatua mbili hadi tatu sahihi zinazoweza kuchukuliwa ili kupunguza athari za janga la asili. Wengi katika kundi hili walitaja hatua sahihi chache na nyingine hazikuwa sahihi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 131 (9.3%) walipata alama hafifu kwa sababu walishindwa kueleza hatua zote tano zinazoweza kuchukuliwa ili kupunguza athari za janga la asili. Watahiniwa walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika. Aidha, watahiniwa 12 (0.9%) waliopata alama 0 walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza tahadhari za kujikinga na madhara yanayoweza kutokea kutokana na majanga ya asili kwa hoja kama kama: *kutojenga nyumba za kuishi katika mabonde na kujenga nyumba zinaweza kustahili tetemeko kama mahema.* Alitaja pia, *kutokata miti* badala ya kutoa hoja sahihi kama

*kutoa elimu kwa jamii, kuunda kikundi cha kuchunguza mabadiliko ya hali ya hewa kuwa na vyombo vya habari.* Kielelezo Na. 12.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili vibaya.

**Kielelezo Na. 12.2**

12 Janga la asili ni matukio yanayotokea na kusababisha hatari au vifo. Mfano wa majanga ya asili ni mafuriko, mvua kubwa, kimbunga, milipuko ya volkano na tetemeko la ardhi.

Zifuatazo ni hatua zinazoweza kuchukuliwa na jamii ili kupunguza athari ya janga la asili endapo litatokea.

Kutokujenga nyumba za kuishi kwenye mabonde. Mara nyingi mafuriko yanapotokea ni kwenye sehemu ambazo ni za mabonde na hatimaye kusababisha uharibu wa mali na vifo.

Kupanda miti kwenye maeneo ya yaliyo wazi ili kupunguza mwendo kasi wa kimbunga kinapotoke. Kwani kimbunga huezua paa na kusababisha kubomoka kwa ~~[illegible]~~ nyumba za kuishi.

Kujenga nyumba za mahema kwenye sehemu ambazo mara nyingi tetemeko linakotokea ili kuepuka uharibifu wa miundombinu pamoja na vifo vya watu. Mfano tetemeko la ardhi lili lotokea Kagera.

Tusijenge nyumba za kuishi au kuweka makazi ya watu karibu na volkano zinazoripuka na kusababisha vifo vya watu pamoja na wanyama wanaoishi maeneo hayo.

Tusikae ~~kaa~~ chini ya miti mirefu wakati wa mvua kubwa, kwani mvua ina pokua inanyesha huambatana na radi. Radi ikodondoka chini huunguza mimea na binadamu kuweza kupoteza uhai wake.

Janga la asili ni hatari endapo litatokea yatupasa kuwa makini na


12 Serikali itoe msaada kwa watu waliopatwa na majanga hayo kwani hupoteza nguvu kazi, kurudisha maendeleo nyuma na kusababisha watoto wa mitaani na mayatima.

**Kielelezo Na 12.2** Sampuli ya majibu yasiyokuwa sahihi

### 2.2.3 Swali la 13: Utawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika

Swali la 13 lilitoka katika mada ya *Utawala na Uchumi wa Kikoni Afrika*, na lililenga kupima nyanja ya uchambuzi. Mtahiniwa alitakiwa kutofautisha mfumo wa utawala wa moja kwa moja na utawala wa mlango wa nyuma uliotumika wakati wa utawala wa kikoloni.

Jumla ya watahiniwa 2,331, sawa na asilimia 44.5, walichagua kujibu swali hili, ambapo watahiniwa 374, sawa na asilimia 2, walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5, ambao ni ufaulu hafifu. Pia watahiniwa 889, sawa na asilimia 47.5, walipata alama kuanzia 6 hadi 10 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 608, sawa na asilimia 32.5, walipata alama kuanzia 10.5 hadi 15, ambao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla watahiniwa walifaulu vizuri katika swali hili kwa kuwa watahiniwa 1,497, sawa na asilimia 80, walipata alama kati ya 6 hadi 15. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama inavyoonekana kwenye Chati Na 13.




**Chati Na. 13:** *Viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 13*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa waliopata kuanzia alama 10.5 hadi 15 waliweza kutofautisha kati ya mfumo utawala wa moja kwa moja na utawala wa mlango wa nyuma kwa hoja nne hadi tano. Majibu yao yalibainisha kwa ufasaha tofauti baina ya mifumo hii kwa kuhusianisha hoja kama: *gharama katika uendeshaji*, *ukatili wa*

*kiutawala, upinzani kutoka kwa Waafrika na matumizi ya viongozi wa kiafrika katika uongozi wa kikoloni*. Kielelezo Na 13.1. ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi.


13. Mfumo wa utawala wa kikoloni; ni mifumo ulioa
nzishwa na wakoloni barani Afrika kwalengo la ku-
watawala waafrika. mfumo wa utawala wa kikoloni
Umegawanyika katika aina ~~tatu~~ nne nazo ni mfumo wa mo
ja kwa moja ambao alitumia mjerumani, mfumo wa mlan
go wa nyuma ambao ametumia muingereza, mfumo wa k
ulisha kasumba ambao ametumia mfaransa na mfumo
wa kuheshimu mila na desturi za kiafrika. Zifuatazo
ni tofauti kati ya mfumo wa utawala wa moja kw-
amoja na mfumo wa utawala wa mlango wa nyuma

Mfumo wa utawala wa mojakwa moja ulikuani-
wakikatili ambapo waafrika walifanyishwa kazi kwala-
zima kwa muda wa masaa 48 lakini mfumo wa utaw
ala wa mlango wa nyuma haukua wakikatili ulizing-
atia haki za binadamu katika ufanyaji kazi.

Mfumo wa utawala wa mojakwa moja ulikuwa
na gharama, kwasababu viongozi wengi walikua ni wa
zungu katika usimamizi lakini mfumo wa mlango
wa nyuma haukua na gharama kwasababu ulitumia
viongozi wa kiafrika katika shughuli zao.

Mfumo wa utawala wa mojakwa moja ulikua na
Upinzani; waafrika waligoma kunyanyaswa katikaut
endaji wa kazi lakini mfumo wa utawala wa mlango
wa nyuma haukua na upinzani kwasababu waafri
ka walisimamiwa na waafrika wenzao katika ufanya
ji kazi wao hivyo hawakunyanyaswa.

Mfumo wa utawala wa mojakwamoja ulidha-
rau mila na desturi za kiafrika kama kuabudu-
miungu, kuongea lugha za asili lakini mfumo wa-
mlango wa nyuma uliheshimu mila na desturi za
kiafrika kwa kuwapa uhuru wa kuabudu na-
kuzungumza lugha zao za asili




13. Mfumo wa utawala wa mojakwamoja uli-
tumia viongozi wengi wakizungu katika usimamiz
i wa shughuli wanazoziendesha lakini mfumo wa.
mlango wa nyuma umetumia wazungu wachach
e viongozi wengi walikua ni waafrika.
Hivyo basi pamoja na tofauti hizo za mf
umo wa utawala wa moja kwa moja na mfumo
wa mlango wanyuma lakini pia ipo mifanano k-
atika mifumo hiyo nayoni yote ilikua ya kingon
yaji na yote ilitumia wazungu.

**Kielelezo Na 13.1:** sampuli ya majibu sahihi

Watahiniwa 608, sawa asilimia 32.5, walipata ufaulu wa wastani, waliweza kutofautisha vizuri lakini walitoa hoja mbili hadi tatu kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha. Aidha, baadhi yao walichanganya hoja ambazo sio sahihi na wengine walirudia kuandika hoja zenye maana moja, na hivyo kuwafanya kupata alama za wastani katika swali hili.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 370 sawa na asilimia 20 waliopata alama kuanzia 0 hadi 5.5 walishindwa kujibu swali hili kwa ufasaha kutokana na kushindwa kuelewa matakwa ya swali. Watahiniwa hawa pia walionesha kukosa maarifa kuhusu Utawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika. Baadhi yao walichanganya maelezo baina ya mfumo wa mlango wa nyuma ambao ulitumiwa na Waingereza na mfumo wa kulisha kasumba uliotumiwa na Wafaransa katika makoloni yao, hivyo kupata alama 0 wa kutoa baadhi ya hoja hizo ni kama *utawala wa moja kwa moja*, *utawala wa mabavu* n.k. Hata hivyo, watahiniwa wengine waliweza kuandika kwa usahihi hoja chache zilizobainisha utofauti baina ya mfumo utawala wa moja kwa moja na utawala wa mlango wa nyuma. Kielelezo Na.13.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa tofauti baina ya mfumo wa utawala wa mlango wa nyuma na mfumo wa utawala wa moja kwa moja.



13 Kutofautisha mfumo wa utawala wa moja kwa moja na utawala wa mlango wa nyuma ulio tumika wakati wa utawala wa kikoloni:

Utawala wa moja kwa moja, huu ni utawala ambao hufanyika ndani ya nchi husika.

Zifuatazo ni tofauti za utawala wa kikoloni moja kwa moja na utawala wa mlango wa nyuma.

Utawala wa moja kwa moja ni ule utawala ambao watawala au nchi inaamua kujitawala kwa nyanja zote yaani kiuchumi na kisiasa na kijamii. Kwa utawala wa mlango wa nyuma ni utawala ambao ni wa kidikteta.

Utawala wa moja kwa moja hauna ubaguzi wa rangi lakini utawala wa mlango wa nyuma, huwa ni wa ubaguzi kwa mfano elimu hutolewa kwa watu wenye uwezo wa juu kiuchumi.

Utawala wa moja kwa moja hauna unyanyasaji miongoni mwao lakini ni utawala wa mlango wa nyuma ni utawala ambao huwa na unyanyasaji miongoni mwa wananchi hao.

Utawala wa moja kwa moja huhamasisha wananchi kufanya kazi kwa ajili ya maendeleo ya nchi husika kwa mfano Tanzania lakini utawala wa moja kwa moja ni utawala ambao haihitaji maendeleo ya mtu mmoja mmoja zaidi yao wenyewe kujiendeleza kiuchumi.

Utawala wa moja kwa moja hutoa fursa ya kuanzisha miradi mbalimbali lakini utawala wa mlango wa nyuma ni utawala usiopenda mtu kuanzisha mradi wowote zaidi yao wenyewe wakoloni:


Kwa hiyo katika nchi ni bora zaidi kutumia utawala wa moja kwa moja kama Tanzania ili kuepuka matatizo na migogoro mbalimbali kuweza kutokea kwa wananchi hao kwa mfano kupoteza maisha kutokana na kutotii sheria za amri ya wakoloni kwa hiyo ni muhimu sana nchi kutumia utawala wa moja kwa moja.

Kielelezo Na.13.2: sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakukidhi matakwa ya swali la kumi na tatu.

### 2.2.4 Swali la 14: Vitangulizi vya Ukoloni Tanganyika Zanzibar na Kwingineko Afrika.

Swali la 14 lilitoka katika mada ya *Vitangulizi vya kikoloni Tanganyika Zanzibar na kwingineko Afrika*, na lililenga kupima nyanja ya tathmini. Swali liliuliza "Mapinduzi ya viwanda yaliyokea katika bara la Ulaya miaka 1760 hadi 1870 yalisababisha kuvamiwa na kugawanywa kwa bara la Afrika". Mtahiniwa katika swali hili alitakiwa kutetea hoja kwa kueleza sababu za wakoloni kuvamia bara la Afrika.

Jumla ya watahiniwa 2,323 (55.3%), walichagua swali hili kati yao, watahiniwa 262 (11.3%) walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5 ambao ni ufaulu hafifu. Watahiniwa 920 (39.6%), walipata alama kati ya 6 hadi 10 ambao ni ufaulu wa wastani na watahiniwa 1141 (49.1%), walipata alama kuanzia 10.5 hsdi 15. Jumla ya watahiniwa 2,061 (88.7%), walipata alama kuanzia 6 hadi 15 ambao ni kufaulu vizuri. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na. 14.




**Chati Na. 14:** *Viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 14*

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 1,141, ambao ni sawa na asilimia 49.1, walikuwa na ufaulu mzuri katika swali hili. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha, na hivyo waliweza kueleza kwa ufasaha sababu nne hadi tano za wakoloni kuvamia bara la Afrika. Baadhi ya hoja ni kama; *kutafuta maeneo kwa ajili ya masoko ya bidhaa zilizotengenezwa katika viwanda huko Ulaya, kutafuta maeneo kwa ajili ya uwekezaji, kutafuta maeneo kwa ajili ya malighafi ya*

*viwanda*. Hii inadhihirisha kuwa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji katika mada hii ulifanikiwa vizuri. Kielelezo Na 14.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

14 Uvamizi ni kitendo cha kuingia eneo ambalo sio lako bila idhini ya mwenye h eneo. Uvamizi wa bara la afrika hiki ni kitendo cha mataifa ya ulaya kuja na kuingia afrika bila idhini ya waafrika. Mapinduzi ya viwanda yaliyotokea bara la ulaya yalisababisha kuvamiwa kwa bara la afrika


Kwanza ni kweli mapinduzi ya viwanda yalipelekea kuvamia na kugawanywa kwa bara la afrika kwani yalipelekea wazungu kuja kwaajili ya:-

Kutafuta malighafi kwaajili ya viwanda vyao; Tukumbuke kuwa mataifa ya ulaya yaliendelea tokea muda kulikuwa na viwanda vingi hivyo kutokana na uwepo wa viwanda vingi malighafi zilipunguka hivyo ikawalazimu kuja afrika kwaajili ya kutafuta malighafi kwaajili ya viwanda vyao huko ulaya h ndio maana walifanya uvamizi katika bara la Afrika.

Kutafuta maeneo ya uwekezaji; Kutokana na uwepo wa viwanda vingi ulaya maeneo ya uwekezaji yalipungua hivyo ikawalazimu kutafuta maeneo ambayo wangewekeza mitaji yao na ndipo wakaamua kuvamia bara la afrika.

Kutafuta masoko; Kutokana na uwepo wa viwanda vingi ~~na~~ bidhaa zilizalishwa kwa wingi, Ili walazimu kutafuta masoko ambapo wangeuza bidhaa zao hivyo ndio maana walivamia bara la Afrika.

Kutafuta maeneo kwa ajili ya makazi ya walowezi; Kutokana na watu la bara la ulaya kutaka kuja na kuwekeza afrika walitafuta pia maeneo ambayo yangefaa kwa makazi ya walowezi ambao watasimamia shughuli zote za uzalishaji mali na pia za kibiashara.



14 Kutafuta wafanyakazi rahisi; Kutokana na
uwepo la viwanda ulaya kulihitajika wafanya
Kazi na wafanyakazi wa kule ulaya walikuwa
wanalipwa gharama kubwa hivyo ikawalazimu
Kutafuta wafanyakazi ambao ni rahisi ndio ma
ana wakavamia bara la Afrika.
Licha ya uvamizi huo waafrika hawa
kuwa tayari kutawaliwa kirahisi na mataifa
kutoka ulaya hivyo walipinga uvamizi huo kw
a lengo la kulinda tawala zao, utamaduni
wao na pia biashara zao.

**Kielelezo Na 14.1** Sampuli ya majibu sahihi ya swali la kumi na nne.

Watahiniwa 920, sawa na asilimia 39.6, waliopata ufaulu wa wastani, waliweza kueleza sababu mbili hadi tatu za wakoloni kuvamia bara la Afrika, Baadhi ya hoja ni kama*; kutafuta maeneo kwa ajili ya uwekezaji na kutafuta maeneo kwa ajili ya malighafi ya viwanda*. Hata hivyo, baadhi ya hoja hazikuwa na maelezo ya kujitosheleza, na hivyo kuwafanya kupata alama za wastani katika swali hili.

Pamoja na ufaulu mzuri katika swali hili, watahiniwa 262, sawa na asilimia 11.3, walifaulu kwa kiwango hafifu. Baadhi ya sababu za kushindwa kwao ni kutokuwa na maarifa katika mada husika au kushindwa kubainisha mahitaji ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliyepata alama 0 aliandika sababu zilizochochea Waafrika kupinga uvamizi wa nchi za Ulaya kuja kutawala bara la Afrika mwishoni mwa karne ya. Kielelezo Na 14.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyokuwa sahihi.

14 Viwanda barani Afrika; ni sehemu ambapo waafrika walikuwa wakizalishia bidhaa zao na kushirikiana na watu wa Ulaya baada ya kuja o wa utangulizi wa wakoloni barani Afrika na kupelekea wakoloni kuja Afrika mnamo karne ya 19 mwa mwaka 1860's hadi 1890's.

Mapinduzi yaliweza kufanywa na waafrika baada ya kunyanyaswa vya kutosha na wakoloni wa Ulaya. Na kupelekea kupingana nao.

Waafrika watetea malighafi zao; kupitia ukoloni uliojitokeza waafrika walijikwamua na kutetea kuchukuliwa malighafi zao amba zo zilikuwa zikiinua viwanda vya Ulaya walipokuwa wakipeleka kuzalisha bidhaa nyingine. mfano wa bidhaa ni dhahabu, chuma.

Waafrika walipinga unyonyaji wa mashamba yenye rutuba, Hali hii ilipelekea waafrika kunyang'anywa na wazungu baadhi ya mashem

14 mba ambayo yalikuwa na rutuba ya kustawi
she mazao kwa ufanisi wote.

Waafrika walipinga na kukomesha Soko la
utumwa, ambapo soko hilo lilikuwa likichu
kua waafrika vijana wenye nguvu na kuuzwa
kupelekwa uleya kwa ajili ya kupelekwa
kuzalisha viwandani uleya.

Walipingana na tamaduni za kigeni walizo
kuwa wakieneza wazungu huku wakiteka
kuwateka, Hali hiyo ilipelekea waafrika
kupingana nayo ambapo nia yao wazungu ni
kupoteza tamaduni za Afrika na kujenga zao
tamaduni za uleya.

Waafrika walimarisha mbinu za kivita na
kijeshi ili kukabiliana na wazungu; Hali hiyo
iliwaogopesha wazungu na kuona kwamba
waafrika nao hawaogopi kukabiliana nao,
baada ya mbinu yao walitumia ya kuwate-
ka kwamba wazungu hawafai na kuchukuli
wa baadae na waafrika kwamba nao wana
kufa waliweza kugomewa.

Kwa kuhitimisha, waafrika walichoshwa
na kuchukuliwa, kunyonywa na kuuliwa pia
kuteswa na wazungu katika eneo ambalo
silo lao. yaani eneo la kigeni Afrika,
ambapo hali hiyo ilipelekea waafrika
kuunda majeshi yao ya kujikwamua na
ukandamizaji na unyonyaji wa kibinadamu.

**Kielelezo Na 14.2**: sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza sababu ambazo hazihusiani na swali la kumi nanne.

## 2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha (Ufundishaji)


Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili ya ufundishaji kutoka katika masomo ya Jiografia na Historia. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu hii, ambapo kila swali lilikuwa na jumla ya alama 15. Kufaulu kwa watahiniwa katika sehemu hii kuligawanyika katika makundi matatu kulingana na alama walizopata. Watahiniwa waliopata alama kuanzia 0 hadi 5.5 walihesabika kuwa na ufaulu hafifu; walihesabika kuwa na ufaulu wa wastani iwapo walipata alama

kuanzia 6 hadi 10. Aidha, watahiniwa waliopata alama kuanzia 10.5 hadi 15 walihesabika kuwa na ufaulu mzuri.

### 2.3.1 Swali la 15: Upimaji na Tathmini

Swali la 15 lilitoka katika mada ya *Upimaji na Tathmini*. Swali lililenga kupima nyanja ya tathmini, na mtahiniwa alitakiwa kueleza faida tano za matumizi ya kumbukumbu za upimaji wa wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji.

Watahiniwa wote 4202 (100%), walijibu swali hili, na kati yao watahiniwa 114, sawa na asilimia 2.7, walipata alama kuanzia 0 na 5.5, ambao ni ufaulu hafifu. Pia watahiniwa 2159 sawa na asilimia 51.4 walipata alama kuanzia 6 na 10 ambao ni ufaulu wa wastani Watahiniwa wengine 1,929, sawa na asilimia 45.9, walipata alama kuanzia 10.5 na 15, ambao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla watahiniwa walifaulu swali hili kwa kiwango kizuri kwa kuwa jumla ya watahiniwa 4,088, sawa na asilimia 97.3 walipata alama kuanzia 6 hadi 15. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na.15.




**Chati Na. 15:** *Viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 15*

Watahiniwa waliopata alama kuanzia 10 hadi 15 walidhihirisha kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu faida za matumizi ya kumbukumbu za

upimaji wa wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji katika somo la Jiografia. Wathiniwa hao pia walielewa vema mahitaji ya swali na hivyo kujibu kwa ufasaha. Vilevile, mada hii hufundishwa katika masomo mengi hivyo ilikuwa rahisi kwa watahiniwa kuhawilisha maarifa kutoka somo moja kwenda jingine. Sababu hizo ziliwawezesha kueleza vizuri faida nne hadi tano za matumizi ya kumbukumbu za upimaji wa wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji. Faida hizo ni kama vile; *kusaidia kuboresha ufundishaji, kuandaa ripoti ya maendeleo ya wanafunzi, kujua changamoto zinazowakumba wanafunzi katika ujifunzaji, kuchochea ari ya kujifunza na kujua kiwango cha uelewa wa wanafunzi*. Kielelezo Na 15.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi.


15. Kumbukumbu za Upimaji; Ni yale mambo-mbalimbali ambayo mwalimu anaweza kurejea pale anapohitaji katika kupima stadi, mwelekeo, na ujuzi mbalimbali. Mfano wa kumbukumbu za upimaji ni alama za majaribio, Mazoezi, Mitihani na hata kazi mradi. Zifuatazo ni faida za matumizi ya kumbukumbu za Upimaji wa Mwanafunzi katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la jiografia, nazo ni:-

Husaidia Kuboresha ufundishaji: Mfano, Alama za jaribio ni moja ya kumbukumbu, Unapotoa jaribio na kuweka kumbukumbu, utaweza kujua ni kiasi gani umeeleweka wakati ulipofundisha, hivyo husaidia kuboresha mbinu za ufundishaji ili kuweka kiwango kizuri cha elimu katika shule husika katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la jiografia.

Husaidia katika uandikaji na utoaji wa ripoti juu ya maendeleo ya mwanafunzi Kitaaluma kwa wazazi au walezi wa mwanafunzi husika juu ya Ufundishaji na ujifunzaji wa somo la jiografia. mfano alama za mtihani.

Husaidia kujua changamoto zinazowakumba katika ujifunzaji wao na kuweza kubuni njia ya kuzitatua. Mfano, kumbukumbu za ushiriki wa Mwanafunzi katika mazingira ya shuleni, unapotoa kazi mradi je hashiriki kwa sababu gani au ni kwanini Ushiriki wa mwanafunzi ni wa kiwango cha chini?.

Husaidia katika kuchochea ari ya kujifunza kwa mwanafunzi: Mfano, Kwa kutumia alama za mtihani unaweza kutoa zawadi kwa aliyefanya vizuri hivyo huwafanya wengine waongeze bidii katika kusoma na kuwa makini wakati wa ujifunzaji.




15. Hifadhi mwalimu kujua kiwango cha uelewa wa wanafunzi katika ujifunzaji na ufundishaji wa somo la jiografia, Kumbukumbu husaidia kujua wameelewa kwa kiasi gani, mfano, alama za mitihani za somo la jiografia, huonesha aliyeshika nafasi ya kwanza hadi ya mwisho.
Hivyo basi Kumbukumbu za Upimaji ni muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la jiografi kwani husaidia mwanafunzi mwenyewe wakati wa kuhama shule na kwa mwalimu kurahisisha kazi yake. ili kutosifanya kwa ngumu.

**Kielelezo Na 15.1:** Sampuli ya majibu sahihi

Aidha, watahiniwa 2,159, sawa na asilimia 51.4, wali0pata ufaulu wa wastani katika swali hili waliweza kueleza faida mbili sahihi za matumizi ya kumbukumbu za upimaji wa wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji. Baadhi yao walichanganya hoja sahihi na zisizokuwa sahihi na wangine walirudia hoja.

Kwa upande mwingine, baadhi ya watahiniwa waliopata ufaulu hafifu (alama kuanzia 0 hadi 5.5) katika swali hili walishindwa kuelewa matakwa ya swali na wengine kukosa maarifa ya kutosha katika mada husika. Hivyo, walieleza hoja chache na zenye maelezo yasiyojitosheleza. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja hoja kama: *kujua mbinu mbalimbali za kuwapima wanafunzi, kuwatenga wanafunzi kimakundi n.k.* Kielelezo Na 15.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kuwasilisha hoja moja kwa usahihi na hoja zilizofuta hazikuwa sahihi.



15 Upimaji ni kitendo cha kutambua ni kwa kiasi gani wanafunzi wameweza kupata maarifa katika kipindi fulani.

Zifuatazo ni faida za matumizi ya kumbukumbu za upimaji wa wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Jiografia:

Kujua maendeleo ya mwanafunzi. Kumbukumbu za upimaji humsaidia mwalimu kujua maendeleo ya mwanafunzi katika ufaulu.

Kujua mada alizofundisha. Kumbukumbu za upimaji zitamsaidia kujua mada alizo-zifundisha kisha kuwapima wanafunzi.

15 Kujua mbinu mbali mbali za kuwapi-ma wanafunzi. Kumbu kumbu za upimaji humsaidia kubadilisha mbinu za kuwa-pima wanafunzi katika kipindi husika.

Kutunga mitihani kuwapima wanafu-nzi kila nyanja. Kumbukumbu za upimaji humsaidia mwalimu kutunga mitihani huku akizingatia nyanja zote za ufundi-shaji na ujifunzaji.

Humsaidia mwalimu kujua wanafunzi wanapendelea kujifunza nini.


Hivyo basi ni muhimu kwa mwalimu wa somo la Jiografia ~~kuttu~~ kuwapima wanafunzi na pia kuhifadhi kumbukumbu za upimaji huo.

**Kielelezo Na 15.2**: Sampuli ya mtahiniwa aliyetoa jibu moja sahihi na mengine yasiyo sahihi.

### 2.3.2 Swali la 16: Misingi ya Kufundishia na Kujifunzia Somo la Historia

Swali la 16 lilitoka katika mada ya *Misingi ya kufundishia na kujifunzia somo la Historia*; na lililenga kupima nyanja ya matumizi. Swali hili lilimtaka mtahiniwa kufafanua stadi tano ambazo mwalimu wa somo la Historia anapaswa kutumia ili kufundisha somo kwa weledi.


Watahiniwa wote 4202 (100%), walijibu swali hili na kati yao, watahiniwa 3,992, sawa na asilimia 93.4, walipata alama kuanzia 0 na 5.5, ambao ni ufaulu hafifu. Pia watahiniwa 206, sawa na asilimia 6.6, walipata alama kati ya 6 na 10, ambao ni ufaulu wa wastani. Hakuna mtahiniwa aliyepata alama kati ya 10 hadi 15, ambao ni ufaulu mzuri. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa kiwango hafifu, kwa kuwa jumla ya watahiniwa 3,992, sawa na asilimia 93, walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kama unavyoonekana kwenye Chati Na. 16.




**Chati Na. 15:** *Viwango vya kufaulu kwa watahiniwa katika swali la 16*.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa waliopata alama kuanzia 0 na 5.5 walishindwa kuelewa matakwa ya swali; Aidha, wengine walionesha kukosa maarifa katika kufafanua stadi tano ambazo mwalimu wa somo la Historia anapaswa kuzitumia ili kufundisha somo kwa weledi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja ya *kuzingatia idadi ya wanafunzi, uelewa wa wanafunzi na umri*

*wa wanafunzi* badala ya kufafanua stadi ambazo mwalimu wa historia anazopaswa kuzingatia ili kufundisha somo la Historia kwa weledi. Kielelezo Na. 16.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu hafifu katika swali hili.




**Kielelezo Na. 16.1:** Sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye alishindwa kuelewa matakwa ya swali.

Aidha, watahiniwa 206, sawa na asilimia 6.6, walipata ufaulu wa wastani katika swali hili. Watahiniwa hawa walitoa hoja ambazo

hazikujitosheleza na baadhi yao walichanganya hoja sahihi na hoja zisizokuwa sahihi. Aidha, wengine walishindwa kutetea hoja zao, insha zao zilikosa utangulizi, ufafanuzi wa hoja kwa ufasaha na hitimishio.

Watahiniwa wanne sawa, na asilimia 0.1, waliopata alama kati ya 10.5 hadi 15, katika swali hili waliweza kufafanua stadi tano kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika walielewa matakwa ya swali. Kielelezo 16.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi.

16. Stadi ni mahiri au uwezo anao-kuwa nao mtu wa kutenda jambo fulani. Stadi huweza kuwa utaalamu au ufundi wa kutumia kitu fulani na kuwa na manufaa. Zifuatazo ni stadi ambazo mwalimu wa somo la Historia anapaswa kutumia ili kufundisha somo kwa weledi:-

Ubunifu; Hii ni stadi ambayo inahusisha uwezo wa kutenda kitu kutoka akilini, mwalimu wa somo la Historia anapaswa kuwa mbunifu kwa kutengeneza vitu au zana mbalimbali ili kufanikisha somo lake kwa ufanisi.

Kujiamini; Mwalimu wa somo la Historia anapaswa kujiamini wakati anapokuwa akifundisha ili kuweza kufundisha kwa weledi somo na hiyo kuwa mvuto kwani wanafunzi watachukia somo.

Vitendo; Mwalimu wa somo la Historia pia anapaswa kuzingatia kufundisha kwa kutumia vitendo na si muda wote kufundisha kwa nadharia kwani wanafunzi wanaweza kushindwa kumuelewa.

Kutatua migogoro; Pia mwalimu wa somo la Historia anapaswa kutumia stadi ya kutatua migogoro kwa lengo la kuweka uwiano katika darasa lake kwani akishindwa kutatua -

16. Migogoro iliyopo hawezi kufundisha somo kwa weledi.

Udadisi na kufikiri kiyakinifu; Hii pia ni stadi ambayo mwalimu wa somo la Historia anapaswa kuitumia kwani kupitia kudadisi na kufikiri huweza kufanya ugunduzi mambo mengi kuhusu somo lake na hatimaye kufundisha kwa weledi.

Kwahiyo; Ni muhimu sana kwa Mwalimu wa somo la Historia kutumia stadi zote katika ufundishaji kwani zina manufaa mengi ili kufanikisha ufundishaji kwa weledi.

**Kielelezo Na. 16.2** Sampuli ya majibu sahihi

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA WATAHINIWA KWA KILA MADA

Mtihani wa somo la Maarifa ya jamii ulikuwa na maswali (16) yaliyotoka katika mada (11) za masomo ya Historia na Jiografia. Kati ya hizo, mada saba (7) ni za somo la Historia na mada nne (4) ni somo la Jiografia.

Uchambuzi wa ufaulu kwa watahiniwa katika mada mbalimbali unaonesha kuwa watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri katika mada saba. Mada walizofaulu vizuri ni: Upimaji na Tathmini, iliongoza kwa asilimia 97.3, ilifuatiwa na Ukombozi wa Bara la Afrika, iliyokuwa na asilimia 88.5 na Mabadiliko ya Kijami, Kisiasa na Kiuchumi katika Afrika Huru kwa asilimia 86.5. Mada nyingine ni Ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika, asilimia 80.9, Utawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika, asilimia 80, Nchi yetu Tanzania asilimia 72.4, na Sayari Dunia.

Hata hivyo, mada tatu zilikuwa na ufaulu wa wastani, ambazo ni Asili na Mabadiriko ya Binadamu na Mazingira, asilimia 68, ikifuatiwa na Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani asilimia 65.5 na Upinzani dhidi

ya Uvamizi wa Kikoloni Barani Afrika, asilimia 45.7. Watahiniwa walikuwa na ufaulu hafifu katika mada moja tu, ambayo ni Misingi ya Kufundishia na Kujifunzia somo la Historia, kwa kiwango cha asilimia 6.6.

Kwa ujumla, watahiniwa wameweza kufaulu vizuri katika mada saba kwa sababu walikuwa na umahiri wa kutosha katika mada hizo. Hata hivyo, watahiniwa walikuwa na ufaulu wa wastani katika mada tatu. Kiwango kizuri cha ufaulu katika mada hizi kinadhihirisha kuwa watahiniwa walifanya maandalizi ya kutosha kwa ajili ya mtihani wa Maarifa ya Jamii. Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa hawakuwa makini kusoma maswali na kuyaelewa. Vilevile baadhi ya watahiniwa hao walionesha kukosa maarifa ya kutosha: na hivyo kushindwa kuelewa matakwa ya swali. Muhtasari wa ufaulu wa watahiniwa kwa mada umeoneshwa kwenye Kiambatanisho A.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa mtihani wa Ualimu Daraja A katika somo la Maarifa ya Jamii mwaka 2019 ulizingatia muhtasari wa somo la Maarifa ya jamii. Maswali yote pia yalizingatia ngazi zote za utambuzi zikiwemo; Nyanja ya maarifa, ufahamu, matumizi, uchambuzi, uundaji na tathmini. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika somo hili kilikuwa kizuri

Uchambuzi huu umebainisha changamoto mbalimbali ambazo hazina budi kutafutiwa ufumbuzi kwa lengo la kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza, na hivyo, kuboresha kiwango cha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Maarifa ya Jamii. Changamoto hizo ni kama; watahiniwa kukosa uelewa wa swali, na kushindwa kutoa majibu sahihi kulingana na matakwa ya swali. Vilevile baadhi ya watahiniwa walikosa umakini na hivyo, kutoa hoja ambazo hazihusiani kabisa na swali husika.

Taarifa hii itasaidia kutoa mrejesho kuhusu namna mada za somo la Maarifa ya Jamii zilivyofundishwa vyuoni, na hivyo kuonesha maeneo yenye upungufu katika ufundishaji na ujifunzaji. Hii itatoa fursa nzuri zaidi kwa wakufunzi, wanachuo, na wakuza mitaala kuboresha ufundishaji na ujifunzaji na hivyo kuboresha ufaulu wa watahiniwa kwa miaka ijayo.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuboresha kiwango cha ufaulu katika somo la Maarifa ya Jamii inapendekezwa kuwa;

(i) Wakufunzi waweke mkazo katika mada zote za Taaluma na Ufundishaji kwenye masomo ya Historia na Jiografia wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Hii itasaidia kuleta uwiano mzuri wa ufaulu katika mada kwenye masomo husika.

(ii) Wakufunzi waweke mkazo katika matumizi ya mbinu shirikishi hususani mbinu ya majadiliano ili kuwajengea wanachuo uwezo mkubwa wa kuwasilisha hoja zao kwa kuongea na kuandika. Hii itawasaidia kujibu maswali ya insha katika mtiririko unaotakiwa na hatimaye katika mtihani wa mwisho.

(iii) Wakufunzi wasisitizie umuhimu wa watahiniwa kuzingatia matakwa ya swali wakati wa mchakato wa kujifunza ili wajenge mazoea ya kujibu maswali kulingana na walichoulizwa. Hii itasaidia watahiniwa wengi kutoa majibu yanayoendana na mahitaji ya swali na kuepuka kuchanganya dhana wakati wa kujibu maswali.

(iv) Mkazo zaidi uwekwe katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada zote kwa kutumia njia shirikishi ili kuwajengea wanachuo umahiri wa kutosha katika mada zote zilizoainishwa katika muhtasari wa somo la Maarifa ya Jamii.

(v) Wakufunzi wawasisitize watahiniwa kuwa watulivu na kusoma kwa makini wakati wa kujibu mtihani kwani baadhi yao huwa na haraka ya kufanya swali bila kutulia na kutafakari kwa kina, na hivyo kukosa maswali kwa uzembe.

KIAMBATANISHO A

**Muhtasari wa Ufaulu kwa Watahiniwa Katika Kila Mada**

<table>
<tr><th rowspan="2">Na</th><th rowspan="2">Mada</th><th rowspan="2">Idadi ya Maswali</th><th rowspan="2">Namba ya Swali</th><th colspan="2">% ya Kufaulu</th><th rowspan="2">Maoni</th></tr>
<tr><th>Wastani wa ufaulu kwa swali</th><th>Wastani wa ufaulu kwa mada</th></tr>
<tr><td>1</td><td>Upimaji na Tathmini</td><td>1</td><td>15</td><td>97.3</td><td>97.3</td><td>Vizuri</td></tr>
<tr><td>2</td><td>Ukombozi wa bara la Afrika</td><td>1</td><td>10</td><td>88.5</td><td>88.5</td><td>Vizuri</td></tr>
<tr><td>3</td><td>Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi katika Afrika Huru</td><td>1</td><td>8</td><td>86.5</td><td>86.6</td><td>Vizuri</td></tr>
<tr><td rowspan="2">4</td><td rowspan="2">Vitangulizi vya ukoloni Tanganyika, Zanzibar na Kwingineko Afrika</td><td rowspan="2">2</td><td>7</td><td>73.1</td><td rowspan="2">80.9</td><td rowspan="2">Vizuri</td></tr>
<tr><td>14</td><td>88.7</td></tr>
<tr><td>5</td><td>Utawala na Uchumi wa Kikoloni Afrika</td><td>1</td><td>13</td><td>80</td><td>80</td><td>Vizuri</td></tr>
<tr><td rowspan="2">6</td><td rowspan="2">Nchi yetu Tanzania</td><td rowspan="2">2</td><td>1</td><td>94.2</td><td rowspan="2">72.4</td><td rowspan="2">Vizuri</td></tr>
<tr><td>11</td><td>50.5</td></tr>
<tr><td rowspan="4">7</td><td rowspan="4">Sayari Dunia</td><td rowspan="4">4</td><td>3</td><td>76.7</td><td rowspan="4">70.8</td><td rowspan="4">Vizuri</td></tr>
<tr><td>4</td><td>62.5</td></tr>
<tr><td>5</td><td>53.5</td></tr>
<tr><td>12</td><td>90.7</td></tr>
<tr><td>8</td><td>Asili na Mabadiliko ya Binadamu Teknolojia na Mazingira</td><td>1</td><td>9</td><td>68</td><td>68</td><td>Wastani</td></tr>
<tr><td>9</td><td>Stadi Sahili na Tata za Picha na Ramani</td><td>1</td><td>2</td><td>65.4</td><td>65.4</td><td>Wastani</td></tr>
<tr><td>10</td><td>Upinzani dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Barani Afrika</td><td>1</td><td>6</td><td>45.7</td><td>45.7</td><td>Wastani</td></tr>
<tr><td>11</td><td>Misingi ya Kufundishia na Kujifunzia somo la Historia</td><td>1</td><td>16</td><td>6.6</td><td>6.6</td><td>Hafifu</td></tr>
</table>